JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU

SIMU 0752547814 P.O.BOX 170 MWANZA

BARUA PEPE bwirugirls@gmail.com

KUMB.BGSS/JIF/01/2019

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……

S.L.P ……

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Mpendwa mwanafunzi……..

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO** mwaka wa masomo **2021/2022** katika shule ya Sekondari Wasichana Bwiru. Mwaka wa masomo utaanza tarehe 18/7/2020 na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 18/7/2020. Tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo.

Mahali shule ilipo

Shule ya sekondari ya wasichana Bwiru iko katika kata ya Pasiansi, Manispaa ya Ilemela Mkoani Mwanza. Shule inafikika kiurahisi kwani kuna usafiri wa magari ya abiria(daladala) kutoka mjini hadi Bwiru. Magari hayo yanapatikana kwenye stendi ya Bwiru iliyoko karibu na soko kuu Mwanza mjini.

Pamoja na barua hii naambatisha orodha ya vifaa muhimu ambavyo lazima uwe navyo, sheria za shule, kanuni za shule ambazo unatakiwa uzifuate kwa muda wote utakaokuwa mwanafunzi wa shule hii, **cheti cha kuzaliwa kama hauna uje na Affidavity . Fomu ya uthibitisho wa afya yako iliyojazwa na daktari wa hospitali ya serikali tu**, fomu ya taarifa binafsi ambazo unatakiwa kuzikamilisha kabla hujafika shuleni, result slip/hati ya matokeo original na fotokopi pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya shule.

Mzazi/mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma/kujaza maelekezo hayo kwa makini ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

.

MecktildaJ.Shija
MKUU WA SHULE

SHERIA ZA SHULE:

Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa asijihusishe na makosa yafuatayo hapa chini vinginevyo anaweza kufukuzwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au mali ya mtu binafsi
8. Kudharau Bendera ya Taifa/wimbo wa Taifa
9. Kuolewa
10. Kupata mimba
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule na jumuiya nzima.
13. Kukataa adhabu /kugomea adhabu
14. Kuingia kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni na katika kumbi za starehe
15. Kulala nje ya shule bila ruhusa
16. Utoro
17. Kutumia au kumiliki simu shuleni.

KANUNI ZA SHULE:

A.*HESHIMA.*

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Kusimama na kumsalimu Mwalimu/mfanyakazi au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
2. Kutotumia lugha mbaya wakati wowote kwa wanafunzi wenzake, walimu/wafanyakazi na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
6. Kuwa na kucha fupi zisizo pakwa rangi, na nywele fupi (kwa asiyependa kusuka) pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbia kuelekea aliko mtu anayekuhitaji (mwalimu/mfanyakazi/kiranja).
8. Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa **"Coat of Arms",** wimbo wa Taifa na fedha, za Taifa.

9. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, ukumbi wa chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma
11. Kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia njema mahali popote ulipo
12. Kunyoosha mkono juu na asimame anapouliza au kujibu swali
13. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya Mwalimu au Kiongozi wa darasani.
14. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta vifaa vya gharama shuleni kama redio, video, simu za mkononi n.k.

B*: MAHUDHURIO:*

Kila mwanafunzi anatakiwa,

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya taifa, mikutano ya nyumba(mabweni) na madarasa.

C. MAANDALIO YA JIONI:

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maaandalio ya jioni **1:30** hadi saa **4:00** usiku.
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.
3. Walimu wa zamu watakuwa wanasimamia maandalio ya jioni kikamilifu.

D. KUWAHI:

Kila mwanafunzi anatakiwa:-

1. Kuthamini muda
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa.

E. SARE ZA SHULE:

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika Sare ya Shule wakati wote wa:-

1. Masomo darasani.
2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
3. Kwenda Hospitali
4. Baraza la shule
5. Anaposafiri kuja shuleni au kwenda nyumbani kwao wakati wa likizo.
6. Kazi za mikono **(vazi la kazi)**
7. Michezo.

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, viatu vyenye visigino virefu, mapambo yoyote pamoja na sare za shule.

F. MIPAKA YA SHULE:

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

1. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu
   a) Ofisi ya walimu (staff room)
   b) Ofisi nyingine za shule
   c) Maabara
   d) Jikoni
   e) Nyumba za walimu/wafanyakazi wasio walimu.

G. UGONJWA:

1. Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika katika /zahanati ya shule na endapo atazidiwa atapelekwa katika **Hospitali** ya **Serikali.**
2. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima amfahamishe **Matron/ Mama malezi** wa shule, mara afikapo shuleni.
3. Wagonjwa wafike Zahanati **saa 1.00** asubuhi kwa ajili ya matibabu kabla ya kwenda darasani.
4. Mwanafunzi aje na bima ya afya (NHIF) inayotumika au aje na Tsh 50,400/= kwaajili ya kukatiwa bima.

<u>MAHITAJI MUHIMU:</u>

A. *ADA*

1. Ada ya shule ……. Sh. 70,000/= (kwa mwaka) au **35,000/=** (kwa muhula) pesa hii ilipwe kwenye akaunti ya shule 31101200105 Benki ya **NMB** Jina la akaunti **Bwiru Girls Secondary School**

b. MICHANGO MINGINE

michango ifuatayo ilipwe kwenye akaunti 31101200024 NMB. Jina la akaunti BWIRU GIRLS SECONDARY SCHOOL FUND

2. Taaluma …… Sh. 20,000/= (kwa mwaka)
3. Ulinzi/upishi/vibarua …… Sh. 30,000/=
4. Tahadhari …… Sh. 5,000/=
5. Afya …… Sh. 20,000/=
6. Ukarabati…… Sh. 15,000/=
7. Mock …….. <u>Sh. 20,000/=</u>
8. Kukodi godoro ……. Sh. 20,000/=

NB: a.Tafadhali unakumbushwa kulipa kwa kuzingatia namba za akaunti ulizopewa.

b. Hapa shuleni hatupokei pesa taslimu, Ada na michango yote elekezi ni lazima ilipiwe Benki isipokuwa pesa ambayo mzazi ameelekezwa kuwa iletwe mkononi tu.

c. Risiti ya malipo halisi(original) iletwe shuleni mwanafunzi atakaporipoti

d) Malipo yote ya bank yaanze kuingizwa tarahe 1/7/2020 na sikabla ya hapo

C. MAHITAJI MENGINE

Pesa hii italipwa taslimu shuleni

1. Kitambulisho cha shule……. Sh. 6000/-
2. Nembo ya shule@……..sh 2000/=
3. Pesa za uniform
4. Pesa za bima ya afya

D. SARE ZA SHULE

1. Sketi mbili nyekundu zikiwa na marinda mapana, ndefu kitambaa cha suti urefu katikati ya magoti na makanyagio (zinapatikana shuleni)
2. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu kitambaa cha cotton
3. Sweta moja nyeusi
4. Tai moja nyekundu yenye mistari mshazali mieupe (inapatikana shuleni)
5. T-shirt moja yenye kola shingoni rangi ya light blue (inapatikana shuleni)
6. Shuka mbili rangi ya light blue na foronya zake
7. Gauni mbili zenye rangi ya light pink ndefu kwenda chini katikati ya magoti na makanyagio (inapatikana shuleni)
8. Track suit nyeusi, viatu raba na jezi nyesu kwaajili ya michezo.
9. Vazi la kiislam linalotumika kama sare ya shule liwe na kitambaa cha kichwani cheupe, (juba) nusu kanzu nyeupe kitambaa cha cotton na suruali nyekundu kitambaa cha suti (inapatikana shuleni)
10. Vazi la kiislamu linalotumika kama nguo ya kushindia (shamba dress) liwe la rangi ya pink. (gauni refu na kitambaa cha kichwani) (inapatikana shule)
11. Viatu vya wazi (sandal) kwakishindia.

ANGALIZO: Mavazi yote inabidi yawe yenye hadhi, ukishindwa kuelewa maelekezo haya unaweza kupata huduma hizo hapa shuleni kwani wapo mafundi wanafanya kazi hizo kwa gharama za kawaida. Soma kiambatanisho cha bei ya sare, sare isiyizingatia maelekezo haitapokelewa

C: VIFAA NA MAHITAJI MENGINE:

1. Chandarua (nyeupe)
2. Ndoo moja ya kuogea. Pia alete chombo cha kuhifadhia maji safi ya kunywa.
3. Vifaa vya usafi binafsi kama pedi, miswaki na dawa, sabuni, mafuta, toilet paper n.k.

4. Vifaa vya kulia chakula – kikombe, sahani, kijiko pamoja na bakuli lenye mfuniko.
5. Ream mbili **(2)** za karatasi **(photocopy paper, - A4).** Mwanafunzi atatakiwa kuleta ream moja kila mwaka – iletwe muhula wa kwanza
6. Soksi ndefu nyeupe zisizo na maua jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na urembo - visigino vifupi , kiwi na brashi.
7. Raba kwa ajili ya michezo.
8. Madaftari makubwa ya kutosha masomo yake
9. Vifaa vya somo la hisabati (Mathematical set), Calculator, graph pad 1 pamoja na **DISECTING – KIT 1** kwa wanafunzi wanaosoma somo la **Biolojia.**
10. Tochi 01 inayotumia mwanga wa jua kwa matumizi binafsi
11. Mashuka ya kutosha, mto mmoja na blanketi moja zito.
12. Godoro futi mbili na nusu kwa sita au la kukodi linapatikana shuleni kwa **Tsh. 20,000/=** kwa mwaka. Pesa hiyo ilipwe benki kwenye akaunti iliyoandikwa kwenye fomu hii. **Godoro lililotumika haliruhusiwi**
13. Nguo za ndani za kutosha kama chupi, gagulo shimizi, skin tight n.k – ziwe nyeupe au nyeusi, taulo, khanga/vitenge
14. Kila mwanafunzi aje na mifagio mitatu **(03)** ya chelewa pamoja na:-

- Jembe lenye mpini - kwa **PCB**
- fyekeo 01 - kwa **CBG na HGE** na **HKL**
- Soft bloom 01 - kwa **HGL**
- Reki 01 - Kwa **HGL na PCM**
- Hard bloom moja - kwa **HGK**
- Ndoo kubwa moja - kwa **EGM**

Kila mwanafunzi aje na ndoo moja ndogo kwa matumizi yake binafsi

Muhimu:

1. Fedha anazotumiwa mwanafunzi akiwa shuleni zitumwe kwa njia ya M-PESA namba ya WAKALA **068456 – PAUL MWITA.** Mzazi akishatuma fedha hiyo atume ujumbe kwenye simu namba(**0755922222)** akiandika jina la mwanafunzi aliyemtumia fedha hiyo, ukionesha jina la mwanafunzi darasa na tahasusi anayosoma. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda BENKI, POSTA/KITUO CHA MABASI kuchukua fedha zitakazotumwa kwa njia hizo. Uongozi wa Shule hautahusika na mihamala ya fedha itakayofanyika kinyume na utaratibu uliotolewa

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma.

NB: Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti shuleni mapema kuanzia saa1**.30** asubuhi mpaka saa **9.30.** jioni. Mawasiliano yote ya kiofisi kwa njia ya simu itumike namba 0752 547 814. Muda wa kazi na siku za kazi tu.

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU.

1. **Sehemu ya Mwanafunzi:**

   Mimi …….. Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha **tano** mwaka …… katika shule ya sekondari ya Wasichana Bwiru na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi.

   Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea. Nitariporiti shuleni kwa muda uliopangwa kila ninapofunga likizo

   Anuani yangu ya kudumu ni:……

   ……

   ……

2: Sehemu ya Mzazi/Mlezi.

Mimi…….. ninakubali mtoto wangu …….. kuchukua nafasi kuingia Sekondari ya Wasichana Bwiru. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule na atafika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kila wakati. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa. Nitahakikisha mwanangu anaripoti shuleni kwa wakati kila muhula shule inapofunguliwa. Anuani yangu ya kudumu ni: …….

……

Iwapo nitahamishwa au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BWIRU

FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

FOMU HII IJAZWE KWA HERUFI KUBWA

SEHEMU A: TAARIFA BINAFSI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI…….
2. TAREHE YA KUZALIWA……
3. SHULE YA MSINGI ALIKOSOMA……
4. SHULE YA SEKONDARI ALIKOTOKA……
5. TAHASUSI/COMBINATION ANAYOSOMA…….

SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

6. JINA LA MZAZI/MLEZI……..
7. MAHALI ANAPOISHI
8. MTAA/KIJIJI…….
9. WILAYA……
10. MKOA……
11. NAMBA YA SIMU……

MEDICAL EXAMINATION FORM

Bwiru Girls' Secondary School

P.O. BOX 170

MWANZA.

……

Ref. No. BGSS/

The Medical Officer

……..

……

……..

Please examine …….. as to her fitness for pursuing advanced Secondary Education at this School.

1. Hemoglobin……
2. P.V.Bleeding……..
3. (a)Sight……..
   (b)Hearing……
4. BloodPressure……...
5. Sickle Cell Test……
6. Deformit……
7. Urine for sugar & Pregnancy test……
8. Epileps……
9. Leprosy……..
10. Heart Examination ……
11. Tumors - breast ……
12. Pulmonary tuberculosis ……
13. Stool for routine Examination ……..
14. Asthma ……
15. Skin diseases ……

Comments ……

……

NAME: …… SIGNATURE …….…… DESIGNATION……

STATION:…… OFFICIALSTAMP ……..... DATE:……

KIAMBATANISHO

SARE ZA SHULE ZINAZOSHONWA HAPA SHULENI NA GHARAMA ZAKE

S/N	AINA YA SARE	KIASI (SH)	IDADI	KIASI JUMLA (SH)
1.	Sketi	16,000/=	2	32,000/=
2.	Gauni la kushindia	17,000/=	2	34,000/=
3.	Hijab ya darasani	30,000/=	2	60,000/=
4.	Hijab ya kushindia	26,000/=	2	52,000/=
5.	T. shirt	10,000/=	1	10,000/=
6.	Tai	4,000/=	1	4,000/=